# 15. MUSA: ANAZALIWA KUKOMBOA WANA WA ISRAELI

**“Alimwita jina lake Musa, na akaswema, ni kwa sababu nalimtoa majina majini ”**

**Shabaha**

Kuonyesha jinsi Mungu alivyomwandaa Musa kuwakomboa watu wake aliowachagua kutoka katika nchi ya Misri.

Yusufu alikuwa amesema kwamba wana wa Israeli wataondoka Misri na kurudi tena Kanaani, lakini miaka mingi ilipita pasipo kutokea lolote. Kwa muda wa miaka 150 au zaidi, jeneza la Yusufu lilibakia Gosheni mpaka watu wakawa na mazoea nalo, kiasi kwamba walisahau mwosia na mafundisho yake. Walitajirika (mstari 7) na kutoka familia ya watu 70 wakaongezeka mno hadi wakawa taifa kubwa.

Baadaye akainuka mfalme mpya **“asiyemjua Yusufu”** (mstari 8).Kutoka kutendewa kama marafiki, wana wa Israeli wakatendewa kama maadui. Farao mpya aliogopa kwamba wana wa Israeli wangeweza kuungana na taifa lingine na kuishinda Misri, kwa hiyo akawafanya kuwa watumwa (mstari 10).Walipata mateso mengi lakini Mungu aliwabariki na kwa hiyo waliendelea kuongezeka.Na kadri idadi yao ilivyozidi kuongezeka ndivyo Farao alivyozidi kuwaogopa, kwa hiyo aliwaagiza kwamba watoto wote wachanga wakiume wazaliwapo wauawe (mstari 22)

Kutoka 1:1 – 14, 22;2, Matendo 7:18 – 29.

### KUZALIWA KWA MUSA:Kutoka 2:1 – 9

Pale katika Misri wakati huu waliishi wanandoa wawili waaminifu wa kabila la Lawi wakiitwa Amrani na mkewe Yokobedi, walikuwa na watoto wawili; Haruni na Miriamu.Kisha mwana mwingine akazaliwa ambaye **“alikuwa mzuri sana”**(Matendo ya Mitume 7:20).Walikuwa wamedhamiria kumwokoa mtoto huyu katika mikono dharimu ya Farao na kwa imani walidharau amri ya mfalme (Waebrania 11:23). Mungu alikuwa pamoja nao na walifanikiwa kumficha akawa salama kwa miezi mitatu.

Ilipokuwa haiwezekani kabisa kumficha mtoto huyo, mama yake alitayarisha kisafina cha nyasi, (matete yaliyofungwa kwa kamba).Akamwacha mtoto katika safina ukingoni mwa maji na Miriamu akangojea karibu na mahali hapo akiangalia ili aweze kupeleka taarifa kwa yale ambayo yangetokea.Binti Farao akielekea mtoni kuoga aliona safina katikati ya matete, alipopelekewa alikifungua, alishangaa kuona mtoto mzuri mchanga (Kutoka 2:6).Musa alianza kulia na hapana shaka machozi ya mchanga yaliugusa moyo wa binti wa mfalme.Alitambua kuwa atakuwa ni miongoni mwa watoto wa Waebrania, na wakati huo huo Miriamu akajitokeza na kuomba amtafute mlezi,aliharakisha kwenda nyumbani kumchukua Yokobedi na kumpeleka mama wa mtoto kwa binti Farao. **“Na binti Farao akamwambia, mchukue mtoto huyu na unifanyie kazi ya kumlea nami nitakulipa mshahara wako”** (mstari 9).Kwa hiyo Yokobedi akamchukua tena mtoto wake na kumlea Musa na akalipwa mshahara na binti Farao kwa kufanya hivyo.

Ni shukrani za kiasi gani aliyokuwa nayo Yokobedi, siyo tu kwa kumpata mtoto wake akiwa hai,bali kwa kupewa tena mtoto hata kama ilikuwa kwa muda wa miaka michache.

Kwa hiyo wazazi waaminifu walipewa thawabu na Mungu. Wanatajwa na mtume Paulo katika Waebrania Sura ya 11 kuwa miongoni mwa mifano ya watu wa imani iliyo kubwa –**“Kwa imani Musa alipozaliwa akafichwa miezi mitatu na wazazi wake kwa sababu waliona kwamba ni mtoto mzuri, wala hawakuogopa amri ya mfalme”**(Waebrania 11:23)

## MAISHA YA AWALI YA MUSA:Kutoka 2:10

Kwa moyo wa shukrani wa ulinzi wa Mungu wa upendo, Yokobedi alimchukua mtoto wake kumlea na kumtunza kwa niaba yake na kwa kadri Musa alivyopata ufahamu akamfundisha habari za Mungu wa Waebrania, Mungu wa Abrahamu,Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo kwa hao ambao ahadi kubwa na nzuri ajabu walipewa.

Mtoto alikua na wakati mwafaka ulipofika alipelekwa kwa binti Farao na akajulikana kama mwana wa binti Farao. Akamwita jina Musa, ikiwa na maana kumtoa majini. Kutoka katika mahakama ya Misri alijifunza maana ya kuwa mwana wa mfalme na akajifunza hekima ya taifa la Misri. Akawa hodari kwa maneno na matendo(Matendo Mitume 7:22) na kuwa kiongozi wa watu. Hata hivyo,Musa hakusahau mafunzo ya awali na mafundisho ya mama yake na baba yake na kwa hiyo hakufuata maisha ya dhambiya wa Misri (Waebrania 11:24 – 27).

## MUSA ANAWATEMBELEA NDUGU ZAKE :Kutoka 2:11 – 14

Musa alipokuwa na umri wa miaka 40 aliondoka katika mahakama ya Farao na kwenda kuwatembelea ndugu zake

wana wa Israeli. Alikuwa Mungu aliyemfanya Musa kwenda na kuona kazi ya ngumu ya ndugu zake,na siku moja akamwona Mmisri akimtenda vibaya Mwisraeli, akamwua yule Mmisri na kuzmika katika mchanga.Siku iliyofuata alipokwenda akawaona Webrania wakipigana wao kwa wao.Akamwambia yule mkosaji, ambaye alimgeukia Musa na kumwambia **"Ni nani aliyekuweka wewe kuwa mkuu wetu na mwamuzi juu yetu?Je wataka kuniua mimi kama ulivyomuua yule Mmisri?"** (mstari 14). Kumbe, Musa akatambua kuwa kifo cha Mmisri hakikufichika kama alivyofikiria. Habari zikaenea haraka sana, Musa akaogopa na akatoroka. Farao aliposikia habari hizi alitaka kumwua Musa, lakini Musa alikuwa amesha toroka kwenda katika nchi ya Midiani.

## MUSA KATIKA MIDIAN:Kutoka 2:15 – 2

Akiwa katika kisima huko midiani Musa alionyesha moyo wa huruma kwa binti saba wa kuhani wa midiani. Alipokelewa katika nyumba yao na baadaye akamwoa Sipora mmoja wa binti hawa saba. Sasa maisha ya Musa yalikuwa tofauti sana na yale ya awali, maisha ya kazi nyingi katika mahakama ya Farao yalibadilika kuwa yale ya mchungaji, yalikuwa maisha ya upweke na magumu, lakini yale ambayo yalimfundisha kumtegemea Mungu. Alijifunza kujali mahitaji ya kondoo wake wadogo na waliozeeka na kuwalinda kama vile ambavyo Mungu alivyokuwa anamlinda yeye.

Katika ukimya aliweza kufikiri juu ya mambo ambayo wazazi wake walikuwa wamemfundisha kama mtoto mdogona pia aliweza kukumbuka mateso ya watu wake katika Misri. Miaka hii arobaini ilikuwa ni muhimu sana kama sehemu ya mafunzo kwake Musa kama ambavyo Mungu alikuwa akimwangalia mtu huyu na kumwandalia kwa kazi maalumu kama ambavyo sasa alikuwa amejifunza kuwachunga kondoo na kuwaongoza, kwa hiyo ingekuwa siku moja aongoze taifa la Israeli kutoka katika nchi ya Misri.

## FUNDISHO KWETU.

Tumeona katika somo hili jinsi mafunzo ya miaka ya awali ya Musa yalivyomwezesha kujitenga kabisa kutoka katika njia za udhalimu katika mahakama ya Farao. Katika Methali 22:6 tunaambiwa: **"Mlee mtoto katika njia ipasayo, naye hataicha hata atakapokuwa mzee"**

Ulimwengu unaotuzunguka sisi ni kama Misri.Mioyo ya watu imejazwa na udhalimu, wanaabudu vitu wanavyoviona karibu yao na hawamjui Mungu wa kweli. Musa angeweza kuwa na heshima kubwa katika mahakama ya Farao na kuishi katika maisha ya anasa katika maisha yake yote, lakini alichagua kuachana na vitu hivyo. Daima alikumbuka ahadi nzuri sana ajabu kuliko heshima na maisha ya anasa -maisha ya uzima wa milele katika Ufalme wa Mungu.

Hebu na tufuate mfano wa Musa na kuyajaza mawazo yetu Neno la Mungu, kisha na sisi kama yeye kwa furaha tutaachana na raha za ulimwengu na kujiandaa kwa wa Ufalme wa Mungu unaokuja.

### MAELEZO YA ZIADA

Maandiko yanatuonyesha jinsi mkono wa Mungu ulivyokuwa unafanya kazi katika maisha ya Musa. Kuanzia namna alivyookolewa kutoka katika kifo alipokuwa mchanga, na kurejeshwa katika ulinzi wa wazazi wake wa familia ya kiebrania wacha Mungu, na kuelimishwa katika mahakama ya Farao na kuwa kiongozi wa watu, tunaona Mungu amwandaa kwa kazi ambayo alimchagua aifanye.

Katika Matendo ya Mitendo 7:25 Stefano alizungumza kwa uvuvio kuhusu matukio haya, akasema **"Yeye(Musa) alifikiri kwamba ndugu zake watafahamu ya kuwa Mungu anawapa wokovu kwa mkono wake"**. Hapana shaka mama yake alimfundisha maneno ya Yusufu. **"Yusufu akawaambia nduguze mimi nitakufa lakini Mungu atawajia ninyi bila shaka atawapandisha kutoka nchi hii, mpaka nchi aliyowaapia Ibrahimu na Isaka na Yakobo"** (Mwanzo 50:24). Akiwa na umri wa miaka arobaini, alifikiri kuwa yuko tayari kuwa kiongozi wao na kumwondoa katika utumwa. Lakini watu hawakuwa tayari kumkubali, na Mungu alijua kwamba Musa mwenyewe alikuwa bado ana mengi ya kujifunza kabla ya kuifanya kazi kubwa ya kuwakomboa. Miaka arobaini zaidi ya kumwandaailihitajika.Mungu alifahamu kuwa maisha ya mchungaji yalikuwa ni mafundisho mazuri sana ambayo Musa alihitaji kuyapata.Kwa njia hii Musa alifanana Bwana Yesu Kristo, **"ambaye ni mchungaji mwema"** (Yohana 10:11) ambaye anawalinda kondoo wake na kuwakomboa katika minyororo (utumwa) ya dhambi na kifo (Waebrania 2:14 – 15)

## MASWALI

### Majibu mafupi

1. Kwa nini Farao aliwafanya Webrania kuwa watumwa?
2. Ni amri gani ya kutisha aliyoiweka Farao?
3. Majina ya baba na mama wa Musa yalikuwa ni yapii?
4. Jina la dada yake Musa ni lipi?
5. Jina Musa lina maana gani?
6. Ni nani aliyemchukua Musa kuwa mwana wake?

7. Musa alikuwa na umri gani alipokimbia kutoka Misri?
8. Kwa nini Musa alikimbia kutoka Misri?
9. Alikuwa akifanya nini katika Midiani?
10. Aliishi katika Midiani kwa muda gani?

**Majibu kwa Kina**

1. Elezea habari jinsi Musa alivyookolewa wakati watoto wote wachanga wanaume wa Waebrania waliuawa
2. Eleza Musa alifanya nini alipokuwa na miaka arobaini
3. Ni njinsi gani maisha ya Musa katika Midiani yalivyomsaidia kujiandaa kuwa kiongozi wa watu wa Mungu

**Majibu ya Ziada**

4. Eleza habari ya Musa kutoka wakati wa kuzaliwa kwake mpaka alipoondoka Misri, wakati alipokuwa na umri wa miaka arobaini.
5. Je unaweza kueleza baadhi ya mambo Musa aliyofundishwa kufanya ambayo yangeweza kumsaidia wakati Mungu alipomwita kuwa mkombozi wa Israeli?